KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

AL-HUDAA [UONGOFU]

الهدى

25/= Ksh

Volume 27

29th Safar 1434

11th Jan, 2013

WASILIANA NASI

SIMU (+254) 721473181
Mombasa, Kenya
E-MAIL Info@qssea.net
Web Site: http://www.qssea.net

YALIYOMO KATIKA JARIDA LA WIKI HII

BID'AH NA SHIRK 1 - 4

HABARI ZA MAZINGIRA YA WAISLAMU KWA MUKHTASAR

MAUAJI MAPYA—TANA RIVER [KENYA] BBC NEWS

Takriban watu 8 wameuawa na wengine kujeruhiwa katika mapigano mapya eneo la Tana River kusini mashariki mwa Kenya.
Taarifa hizi ni kwa mujibu wa shirika la msalaba mwekundu

Mamia waliuawa mwaka jana katika mapigano mengine ya kikabila katika eneo hilo.

Wawili kati ya watu wanane waliouawa wanaaminika kuwa washambuliaji walioshambulia kijiji cha Orma usiku wa kuamkia leo.

Watu wengine watatu walijeruhiwa vibaya , kwa kukatwa katwa na mapanga. Inaarifiwa kuwa hali ni ya wasiwasi huku kukiwa na tetesi za kufanya mashambulizi ya kulipiza kisasi.

Polisi mmoja alithibitisha kuwa watu wanane waliuawa , tisa kujeruhiwa na kuwa nyumba ziliteketezwa wakati wa mashambulizi hayo.

Duru za polisi zilisema kuwa wale waliouawa ni watu kutoka jamii hizo mbili. Na idadi yao imefikisha idadi ya waliouawa tangu kuanza kwa mashambulizi haya ya kuvizia kati ya jamii hizi hadi watu 140.

Ni Chini ya miezi miwili kabla ya uchaguzi mkuuu kufanyika Kenya kwa mara ya kwanza tangu uchaguzi wa

(Endelea Uk. 4)

MJADALA WA KINA KUHUSIANA NA BID'AH NA SHIRK

NA: SHEIKH MUHAMMAD SAALIH AL-MUNAJJID

SUALI: Jee, twaweza kuwaita watu wanaofanya Shirk na Bid'ah Waislamu?

JAWABU: Katika suala hili kuna mas'ala sampuli mbili ndani yake, Bid'ah (Uzushi) na Shirk (Ushirikina; kumfanya Allaah kuwa na washirika).

A. Bid'ah: Suala hili linaweza kugawanyika kwenye Madda Tatu:

1. Maana ya Bid'ah.
2. Orodha za Bid'ah.
3. Hukmu juu ya mwenye kufanya Bid'ah - iwapo hilo linaweza kumfanya yeye kuwa ni kafiri au Laa.

1. Maana ya Bid'ah.

Sheikh Muhammad Ibn 'Uthaymeen (رحمه الله) amesema: "Kulingana na Shari'ah, maana yake ni kumuabudu Allaah kwa njia ambazo Allaah hakutuletea sisi." Ukipenda unaweza kusema, 'Kumuabudu Allaah kwa njia ambazo sizo alizotuletea Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم), wala si njia za Makhalifa wake walio ongoka [*al-khulafaa' ar-Raashidoon*].'"

Taarifa hii ya kwanza imetokana na tafsiri ya Aya: **"Oh! wana washirika (wa Allaah) waliowawekea dini asiyoitolea Allaah ruhusa (yake)?** [Ash-Shuura 42:21]

Taarifa ya pili imetokana na hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), aliyesema: *"Nawasisitiza mimi mushikamane na njia yangu (Sunnah) na njia za Makhalifa wangu walio ongoka katika njia ya sawa [al-khulafaa' ar-Raashidoon] watakaokuja baada yangu. Shikamaneni nayo kisawasawa na muyaume kwa magego yenu (yaani; shikamaneni nayo mafunzo yangu kisawasawa), na mujihadhari na mambo ya kuzua."*

Kwahivyo mtu yoyote mwenye kumuabudu Allaah kwa njia ambayo Allaah hakuiteremsha, au kwa njia ambayo haikufundishwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), wala Makhalifa wake waongofu *[al-khulafaa' ar-Raashidoon]*, atakuwa ni mzushi huyo. Ni sawa iwapo Ibada hiyo ya uzushi itahusiana na Majina na Sifa za Allaah, au zitahusiana na Hukmu zake na Sheriya. Ama kuhusiana na mambo ya kawaida za ki-mila na mazoeya, basi hayo hayaitwi kuwa ni bid'ah (uzushi) katika Uislamu, hata kama ingawa yanawezekana kusifiwa kwa sifa hiyo kulingana na misingi ya ki-Lugha. Lakini kihakika hayo si mambo ya uzushi kulingana na misingi ya Dini, na haya siyo yale aliyotutahadharisha nayo Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Na katika Uislamu hakuna kitu kiitwacho *bid'ah hasanah* (Bid'ah nzuri)." [Majmoo' Fataawa Ibn 'Uthaymeen, Vol. 2, Uk. 291].

2. Orodha za Bid'ah.

Bid'ah inaweza kuorodheshwa kwenye makundi mawili:

(i) Bid'ah inayoweza kumtia mtu kwenye *Ukafiri*.
(ii) Bid'ah isiyoweza kumtia mtu kwenye *Ukafiri*.

Ukiuliza suali: "Ni nini maana ya bid'ah inayoweza kumtia mtu kwenye Ukafiri, na bid'ah isiyoweza kumtia mtu kwenye Ukafiri?

JAWABU: Sheikh Haafidh al-Hukami (رحمه الله) amesema: "Sampuli ya Bid'ah inayoweza kumtia mtu kwenye Ukafiri ni ni pale mtu anapokanusha mas'ala ambayo yaliyoafikiwa na wanavyuoni wote, yenye kujulikana na kila mtu, na ambayo hapana Muislamu yoyote atakaekuwa na sababu ya kutoyajua mas'ala hayo, kama vile kukanusha kitu ambacho ni waajib, kukifanya kitu kuwa ni waajib ambacho si waajib, au kuhalalisha kitu ambacho si halaal au kuharamisha kitu ambacho si haraam;

(Endelea kwenye Uk. 2)

(Endelea Kutoka Uk. 1)

au kuamini baadhi ya dhana zisizomstahiki Allaah, Mtume wake au Kitabu chakehaliyakuwa wote wameepukana na hayo, sawa iwapo dhana hizo zitahusiana na ukanushaji au kukiri—kwa sababu maana yake kuikanusha Qur'an na kuukanusha ujumbe ambao Allaah alioutumiliza nao Mtume wake (صلى الله عليه وسلم).

Mfano wa hayo ni bid'ah ya Jahmiyyah, wanaokanusha Sifa za Allaah, au fikra yakwamba Qur'an ni kiumbe cha Allaah; au fikra yakwamba baadhi ya sifa za Allaah zimeumbwa; au bid'ah ya Qadariyyah wenye kukanusha 'Ilmu na Vitendo vya Allaah; au bid'ah ya Mujassimah waliomfananisha Allaah na viumbe vyake, *na kadhaalika ...*

Orodha ya pili ni bid'ah isiyoweza kumtia mtu kwenye *Ukafiri* imefahamika kuwa ni bid'ah isiyoashiriya kuikanusha Qur'an wala kitu chochote ambacho Allaah alichowatumiliza Mitume Yake.

Miongoni mwa mifano ni bid'ah za Marwaan (alikosolewa na Maswahaba wakubwa, ingawa hawakuwakosoa kama Makaafir au kukataa kuwapa baiy'ah kutokana na bid'ah hizo), kama vile kuchelewesha baadhi ya nyakati za swala mpaka mwishoni mwa wakati wa kisheriya; kutoa khutbah ya 'Eid kabla ya kuswali swala ya 'Eid; kutoa khutba haliyakuwa amekaa katika khutbah ya Ijumaa, *na kadhaalika.* [*Ma'aarij al-Qubool, 2/503-504*].

3. Hukmu juu ya mwenye kufanya Bid'ah - iwapo hilo linaweza kumfanya yeye kuwa ni kafiri au Laa.

Jawabu ni kwamba hilo litategemea. Ikiwa bid'ah yenyewe itasababisha Ukafiri, basi mtu huyo ataangukia kumojawapo mwa sampuli mbili:

(i) Emma inajulikana yakwamba niya yake ni kuisambaratisha misingi ya Uislamu na kuwafanya Waislamu wawe na shaka na Dini yao. Hapana shaka yakwamba mtu sampuli hiyo anakuwa ni Kaafir; kwa hakika yeye ni mgeni katika Uislamu na ni miongoni mwa maadui wa Imani.

(ii) Au iwapo atakuwa amedanganywa na kushawishiwa; hatoweza kushutumiwa na kutangazwa kuwa ni Kaafir mpaka aangaziwe na kudhihirishiwa dalili dhidi yake, kwa njia ya sawa tena iliyo wazi kabisa.

Iwapo bid'ah haikusababisha Ukafiri, basi haifai mtu huyo kushutumiwa kuwa ni Kaafir. Bali, atabaki kuwa ni Muislamu, ingawaje atakuwa amefanya kitendo kiovu kabisa.

Iwapo utauliza, "Sasa tukabiliane vipi na wanaofanya bid'ah?"

JAWABU ni kwamba: Sheikh Muhammad Ibn 'Uthaymeen (رحمه الله) amesema: "Katika hali zote hizo mbili itatubidi kuwaitisha watu hao - wanaodai kuwa wao ni Waislamu, lakini wakawa wanafanya vitendo vya bid'ah zenye kusababisha ukafiri au chini ya hapo - kwenye haki, kwa kuwafafanulia haki ilivyo bila ya kufanya uhasama au kulaumu waliyokuwa wakiyafanya. Lakini pindi tu tutakapotambua yakuwa yakwamba wao ni wapindanifu na kufanya jeuri katika kukubali haki - kwani Allaah amesema: **"Na wala msiwatukane ambao huabudu asiyekuwa Allaah ikawa ni sababu ya wao kumtukana Allaah kwa ujinga."** [*al-An'aam 6:108*]. Na iwapo tutagundua yakwamba wao ni wapindanifu na wafanyao kiburi, basi ni lazima tuwatajie upotofu wao, kwa sababu katika kuwatajia upotofu walio nao unakuwa ndio wajibu wetu juu yao.

Ama kuhusiana na kuwakata na kujitenga nao, hilo litategemea juu ya bid'ah yenyewe waliyokuwa nayo. Ikiwa ilikuwa ni bid'ah yenye kusababisha ukafiri, basi inakuwa ni waajib kumkatilia mbali na kujitenga na mwenye kufanya hayo. Lau kama itakuwa bid'ah yenyewe ni ya daraja ya chini kuliko hapo, basi inakuwa ni wajibu kuzidi kufanya upelelezi. Lau kama itapatikana sahali kutokana na vikwazo juu ya mwenye kufanya hiyo bid'ah, basi tutamwekea vikwazo; na kama hakutopatikana natija yoyote, au ikiwa vikwazo vitamzidisha ku'asi na kufanya jeuri, basi itatupasa kujiepusha na kufanya hivyo, kwa sababu chochote kisicholeta natija nzuri, ni bora kuwachana nacho. Na vilevile, kimsingi, ni haraam kumuwekea vikwazo mu'min yoyote, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Ni haraam kwa Mtu kumkata (kumnymazia) ndugu yake kwa zaidi ya (siku) tatu."* [Yamepatikana kutoka katika *Majmoo' Fataawa Ibn Uthaymeen Vol. 2, Uk. 293*]

B. *Shirk,* sampuli zake na Ufafanuzi

Amesema Sheikh Muhammad Ibn 'Uthaymeen: "*Shirk* ni sampuli mbili; *Shirk* kubwa ambayo ni yenye kumtoa mtu nje ya boma la Uislamu, na *Shirk* ya daraja ya chini ya hapo.

Sampuli ya kwanza, *Shirk* kubwa, ni "Kila aina ya *Shirk* ambayo Muweka Sheriya aliyoieleza kuwa hivyo na ambayo ni yenye kumtoa mtu kwenye boma la Dini yake" - kama vile kujitolea kufanya kitendo chochote cha Ibada kinachostahili kufanyiwa Allaah kwa asiyekuwa Allaah, kama vile kuswali kwa ajili ya kiumbe mwengine badala ya kuswali kwa ajili ya Allaah, kufunga saumu kwa ajili ya asiyekuwa Allaah au kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allaah. Vilevile, ni sampuli ya *Shirk* kubwa kuomba Du'aa' ka asiyekuwa Allaah, kama vile kuwaita walio makaburini au kumwita kiumbe asiyekuwa na wewe (emma aliyekufa au aliye sehemu za mbali) akusaidie kwa njia fulani ambayo hapana mwengine awezae kukusaidia isipokuwa Allaah.

Sampuli nyengine ni *Shirk* ndogo, yenye maana ya kila aina ya maneno au kitendo ambacho Uislamu ulio-orodhesha kuwa ni miongoni mwa Shirk, lakini ikawa haiwezi kumtoa mtu nje ya boma la Uislamu - kama vile mtu akiapa kwa kitu chochote kinyume cha kuapa kwa jina la Allaah, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema yakwamba mtu yoyote mwenye kula kiapo kwa kitu chochote kinyume cha Allaah atakuwa na hatia ya *Kufr* au *Shirk*.

Mwenye kuapa kwa kitu chochote kinyume cha Allaah, lakini akawa haamini yakwamba mtu yoyote asiyekuwa Allaah ana Utukufu sawa na ule wa Allaah, atakuwa ni mushrik aliye na hatia ya shirk ndogo, bila ya kujali iwapo yule aliyemuapia kwa jina lake ametukuzwa na watu au laa..

Hairuhusiwi kuapa kwa jina la Mtume (صلى الله عليه وسلم), au kwa jina la Rais, au jina la al-Kaabah, au kwa Jibreel, kwa sababu hii ni Shirk, lakini ni shirk ndogo isiyoweza kumtoa mtu nje ya boma la Uislamu.

Sampuli nyengine ya Shirk ndogo ni kujinyesha (kufanya vitendo ili watu wakuone) yenye maana ya mtu kufanya kitendo ili watu wakione, na wala sio kwa ajili ya Allaah.

Njia ambazo huku kujionyesha hufutilia mbali vitendo vya Ibada ni miongoni mwa yafuatayo:

YA KWANZA: Ni pale inapotumika kwenye kitendo cha Ibada zenye kudhihirika [*yaani;* mtu yule hafanyi kitendo hicho kwa sababu nyengine yoyote isipokuwa ni kujionyesha tu]. Katika hali hii, kitendo hicho huwa hakifai na ni chenye kukataliwa, kutokana na hadeeth ya Abu Hurairah (رضي الله عنه) iliyonasibishwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), isemayo yakwamba

(Endelea katika Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): “Mimi nimejitosheleza kiyasi cha kwamba sina haja ya kuwa na mshirika. Kwahiyo, yoyote mwenye kufanya amali kwa ajili ya kiumbe mwengine pamoja na Mimi atapata yakwamba Mimi kitendo hicho ni mwenye kumkatalia yule aliyenishirikisha nae.” [Imesimuliwa na Muslim, *Kitaab az-Zuhd, No. 2985*].

YA PILI: Ni pale ambapo kule kujionyesha hutokea baadae wakati mtu anapofanya Ibada [*yaani;* asili ya kitendo kwanza kilikuwa ni kwa ajili ya Allaah, kisha kujionyesha kukaanza kunyapa na kuchukuwa mkondo]. Huwenda ikawa ni kutokana na mojawapo ya hali mbili:

Ya kwanza ni pale mtu anapojaribu kulizuiya lisiwe hivyo - hili halimdhuru yeye.

Kwa mfano, mtu ameshaswali raka’ah, kisha baadhi ya watu wakaja alipokuwa anaendelea na swala yake, mara akarefusha kitendo cha rukoo’ au sujood, au akaanza kujiliza, *na kadhaalika*. Iwapo atajaribu kujizuiya na hilo, haitomdhuru chochote, kwa sababu atakuwa amepambana na fikra hiyo ya kujionyesha. Lakini iwapo ataendelea na hayo ya kujionyesha, basi kila kitendo kitakachotokana na fikra hizo kitakuwa hakifai, kama vile kurefusha kisimamo chake na sijda yake, au akajifanya analiya kwa machozi - vitendo vyote hivyo vitakataliwa. Lakini jee, kukataliwa huku kutaendelea kwenye kitendo chote cha Ibada yote au laa?

Tunajibu yakwamba ni lazima litokee lolote katika yafuatayo:

Ema mwishoni mwa kitendo hiki cha Ibada imeungana na mwanzoni mwake (pasi na kusimama); kwahivyo iwapo mwishoni mwake ilikuwa haifai basi Ibada yote itakuwa haifai kitu.

Hii ndiyo hali ilivyo na swala - sehemu yake ya mwisho haiwezekani kuharibika bila ya kuharibika sehemu yake ya mwanzo, kwahiyo swala nzima itakuwa imeharibika.

Au kama mwanzoni mwa kitendo imegawanyika kutokana na mwishoni mwake, basi sehemu yake ya kwanza itakuwa imekubalika lakini sehemu ya mwisho itakuwa imeharibika. Chochote kilichokuja kabla ya kujionyesha itakuwa sawa, na kilichokuja baada yake kitakuwa hakifai.

Mfano wa hayo ni mtu mwenye riyaal 100, na akatoa swadaka riyaal 50 kwa ajili ya Allaah tena kwa niya iliyotengenea (nzuri), kisha akatoa swadaka riyaal 50 kwa ajili ya kujionyesha tu. Sasa riyaal 50 za mwanzo zimekubalika kama kitendo cha Ibada, na riyaal 50 za mara ya pili zitakuwa zimekataliwa, kwa sababu za kwanza zimegawanyika kando na za pili. [*Majmoo’ Fataawa wa Rasaa’il Ibn ‘Uthaymeen, na al-Qawl al-Mufeed Sharh Kitaab at-Tawheed Vol. 1; Uk. 114, 1st edition*]

ADABU ZA MZAHA KATIKA UISLAMU

NA: THE QUR’AN AND SUNNAH SOCIETY OF EAST-AFRICA

Ibadu Allaah! Moja ya ishara ya utukufu na ukamilifu wa Dini hii nikuwa haikuwa lolote katika mambo ya kimaisha bila ya khutubiwa. Imeweka sharia na maadili ambayo watu ni lazima washikamane nayo na kuishi nayo. Yote hayo kwa Amri za Allaah na matendo ya Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم)

Yaaminiwa na wengi miongoni mwa wasiokuwa Waislamu na kwa masikitiko makubwa pia baadhi ya Waislamu kuwa Uislamu ni dini ya unyanyasaji na ukali, ambapo kucheka, mzaha, kujistarehesha, na machezo ya furaha hayaruhusiwi. Wakati hili likieleweka kwa wasiokuwa Waislamu kufikiria hivi, kwa ujinga wao kuhusu Uislamu, au sura iliyoharibiwa ya Kiislamu, ionyeshwayo daima na vyombo vya mawasiliano, kinachogutusha na balaa, ni pale tunapokutana na Waislamu walio na fikra kama hizo. Enyi Waislamu Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) imebainisha suala hili na kisha yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) ameweka mfano ulio mzuri sana kwa mfumo wa maisha ya Muislamu, kwa wanaotaka kuishi kulingana na al-Hudaa (uongofu). Ukiregea katika Sunnah, twaona kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa Akifanya mzaha na Maswahaba zake, Abu Daawood na Tirmidhi wamepokea kuwa mtu alikuja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akasema: “nipe hayawani wakupanda” Mtume (صلى الله عليه وسلم), Akamjibu: “Nitakupa mwana wa ngamia wa kike” yule mtu akasema kwa mshangao “nitafanyia nini mwana wa ngamia wa kike” (yaani akifikiria kuwa atapewa ngamia mdogo sana wa kupanda). Hapo basi Mtume (صلى الله عليه وسلم), Akamjibu: “Ngamia wa kike wazaa nini isipokuwa ngamia?” (yaani kila ngamia hata akiwa ni mkubwa asili yake ni kuwa ametokamana na mamake).

Tabaraani alipokea kuwa mwanamke mzee alikuja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Akasema: “Ya Rasulla Allaah, niombee Mola wako aniingize Jannah.” Akamjibu: “Jannah haiingiwi na wanawake wazee”, kisha akenda zake kuswali. Aliporegea mke Wake na Mama wa Waumini Aishah (رضي الله عنها) akasema: “Mwanamke mzee aliliona ulilolisema kuwa ni zito mno kwake.” Akajibu: “Allaah Atawabadilisha wanawake wote wakuingia peponi kuwa wadogo wa umri mzuri kabla ya kuwaruhusu kuingia humo.”

Imaam al-Bukhari ametaja katika kitabu chake Al-Adab Al-Mufrad, “Maswahaba walikuwa wakicheza kwa kutupiana maganda ya Matikiti [Watermelon], lakini ulipokuja wakati wa kuwa serious walikuwa waume wa kikweli.”

Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa na adabu ya hali ya juu, kiasi cha kwamba alikuwa mara nyingi akifanya mzaha na kuwachezea watoto. Anas (رضي الله عنه) Alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifanya mzaha alikuwa akimuita ndugu yangu mdogo: “Ewe Abu ‘Umayr! (jina la mchezo) amekuwaje kidege chako? (kidege alichokuwa akikifuga) (al-Bukhari)

Wakati mmoja Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) walimuuliza “Wafanya mzaha nasi?” Akawajibu (صلى الله عليه وسلم) “Ndio, lakini nasema yalio ya kweli.” [Tirmidhi na Bukhari katika Al-Adab Al-Mufrad)

Waja wa Allaah! Yote niliyo yataja ni sehemu ndogo tu wa mzaha Wake (صلى الله عليه وسلم) na Maswahaba. Sitaki kuyapanuwa mno haya kwa sababu ilikuwa na haja ya iwe ni muqadimmah ya mada ambayo ni: ‘Adabu za Mzaha’. Nduzangu katika Imani! Kama mlivyo soma, Uislamu haukatazi kuchezeana na kufanyiana mzaha, lakini imeweka mizani yake, kama alivyotuamrisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) ambayo ni –

1- **KUSEMA UKWELI PEKE YAKE:** Tukiangalia hadithi zilizotajwa juu, Yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwahi kusema neno ambalo halikuwa si la kweli, kama katika kisa cha Ngamia na mwanamke mzee. Hivi ndivyo mzaha unavyofaa kuwa, bila kudanganya, kuzusha, na kuunda ngano ili tu watu

(Endelea kutoka Ukurasa 3)

wacheke. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alionya kuhusu hili: "Ole wake yule ambaye anayedanganya watu basi tu kuwachekesha. Ole wake, Ole wake" (Abu Daawood na Tirmidhi).

2- **ISIHUSISHE AYA ZA QUR'AAN, MANENO YA MTUME (صلى الله عليه وسلم) AU MISINGI YA KIISLAMU YOYOTE.**

Kwa masikitiko wengi wameangukia katika mambo haya yalio mabaya sana. Twamuomba Allaah Awaongoze. Watu hawa watoa mizaha juu ya Malaika, Mitume, na Aya za Qur'aan na hadeeth za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Hili ni jambo la hatari mno kwa kuwa latia dosari katika Imani—Shaykh Al-Utahaymeen (رحمه الله) Alisema: "Yule anayefanya mzaha na Allaah (سبحانه وتعالى), Aya Zake, na Ishara Zake, au Mtume Wake ni kafiri kwa sababu kitendo chabatwilisha Itikadi (Imaan) vipi mtu afanye mzaha kwa analoliamini? Hakika anayeamini jambo alitukuza na kuipa heshima kwa kulifanya jambo hilo liwe mahali pakubwa katika moyo wake. Kufr ni ya sampuli mbili, kukataa, au kupa-mgongo, katika haki na kupinga haki. Yule anayefanya mzaha na dini huwa anatenda kufr ya aina ya pili na matendo yake ni mabaya zaidi ya wale wanaosujudia masanamu. Hili ni suala la hatari mno; mtu anaweza kutamka kilma ambacho kitawapa uzito mkubwa na matokeo katika maangamizo yao. Waweza kutamka kilma kisababishacho adhabu ya Allaah (سبحانه وتعالى) ikawateremkia, na isababishayo kuwaingiza Jahannam. Anaefanya mzaha wa swala, hata ikiwa walikuwa wakifanya mzaha tu, Zakaah, Saumu, au Hajj atakuwa kaafir kwa ijmaa' ya wanazuoni. Vile-vile anayefanya mzaha na ishara za Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kusema kwa mfano, kuwa na msimu wa baridi hakuna busara' au kwa kusema kuwa na upepo msimu wa kiangazi ni upuzi, huyo ni kafiri, kwa sababu matendo yote na Kuumba kwa Allaah yanafanywa na ilmu na hikmah iliyo kamili.

Wakati wa *ghazwah* (vita) vya Tabook, Akiwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amepanda hayawani wake vitani, baadhi ya wanafiki walitamka maneno ambayo yalikuwa na matokeo mabaya juu yao, ingawa walidai baadae kuwa walikuwa wakifanya mzaha tu, Allaah (سبحانه وتعالى) akateremsha Aya zisomwazo mno na Waislamu wote ulimwenguni.

Aliyataja hayo Imaam Ibn Katheer katika Tafseer yake ya Qur'aan, kuhusu Aya ambayo Allaah Asema:

[ATAWBAH 9 : 65 -Na ukiwauliza wao,kwa hakika watasema: "tulikuwa tukiongea na kucheza tu; Sema, "Ni Allaah na Aya zake na Mtume Wake mwafanya Mzaha?]

Imaam Ibn Katheer alisema: "Muhammad Ibn Ka'ab (رضي الله عنه) alihadithia kuwa mtu miongoni mwa wanafiki alisema: "Waliohifadhi Qur'aan wana matumbo makubwa, ni warongo wa ina mbovu mno, na mioga wakubwa wakati wa vita'. Hili lilifikishwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwahivyo wanafiki wakafululiza kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na wakampata amepanda juu ya Ngamia wake. Akasema 'Ya rasulla Allaah nilikuwa nikifanya mzaha tu'. Hapo Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasoma Aya inayosema:

[ATAWBAH 9: 65-Na ukiwauliza, wanasema sisi tulikuwa tukipiga porojo na kucheza tu. Sema: mlikuwa mkimfanyia maskhara Mwenyezi Mungu na aya zake na Mtume Wake 66-msitoe udhuru; mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu! Tukisamehe kundi katika nyinyi Tutawaadhibu wengine kwa kuwa walikuwa wakhalifu]

Mnafiki alikuwa amemshika ngamia wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na miguu yake ikawa yapiga mikiki mawe katika ardhi, ikiyafanya hayo mawe kuruka pande mbali mbali, (kama mpira) kwa mwendo wa kasi aliokuwa aenda ngamia. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa juu ya Ngamia wake hata hakuwa akimuangalia yule mnafiki, ingawa mnafiki, alikuwa ameshikilia mapando na akiwa daima aregelea akisema nilikuwa nafanya mzaha tu!"

Huu ni ushahidi mkubwa kuonyesha kuwa kufanya mzaha na lolote katika Shari'ah, ni hatari kubwa kwa Imaani ya mtu.

Waja wa Allaah! Tunapozungumza kuhusu mzaha, ni lazima tusisitize juu ya suala hili hatari ambalo baadhi ya watu wagusa, ema kwa kujua au kutojuwa, ambayo ni kufanya mzaha na yanayohusika na dini ya Allaah (سبحانه وتعالى) baadhi ya watu wabuni mizaha kuhusiana na haya, na zaidi baadhi ya magazeti wanafanya haya kwa kupitia sehemu za vibonzo vyao. Tumeshataja hukumu ya Uislamu kuhusiana na haya, kwa watu wawe na khofu yamatokeo ya hayo. Tu mara zote tukikumbuka maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)

(Mja wa Allaah aweza kutamka neno, bila yakuwa na mazingatio kuhusu hilo, ambalo neno hilo lamridhisha Allaah na ambalo matokeo yake ni Allaah Apandisha daraja yake Peponi; na Mja wa Allaah aweza kutamka neno, bila ya kuzingatia jambo lenye kumkasirisha Allaah ambalo ni lenye kumsababishia yeye kushuka chini katika Jahannam (Bukhari)

Na katika riwaya nyingine alisema (صلى الله عليه وسلم): "mtu aweza kusema neno bila ya kulizingatia ikamfanya yeye kushuka chini katika Jahannam zaidi ya umbali wa mashariki na magharibi." (Muslim)

1- Kipimo chengine cha mzaha kuruhusiwa nikuwa usimdhuru mtu ikiwa ni kiwili wili au hisia. Allaah Asema:

ALHUJURAAT 49:12. Enyi mlioamini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je! Yupo katika nyinyi anaye penda kuila nyama ya nduguye aliye kufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu.

Ni kwa sababu mambo haya yawaumiza watu haswasiya zao (feelings-hisiya) na yaweza kuumizwa hata kimwili, ikawa Allaah Amekataza. Siku hizi watu wapita mipaka chini ya hadaa ya mzaha. Yasikitisha kuona kuwa baadhi ya watu wapenda kufufua mada ambazo zitawakasirisha ndugu zao wakiwachezea, na hili lawapelekea ndugu zao kuudhika na hata ikawa sababu ya kupigana na kuumizana hata Kifo.

2- Kipimo cha mwisho cha kuruhusiwa kwa mzaha ni kuwa watu wasifanye kupita kiasi, hili lawapelekea wao kukosa hishima zao na kufanya makosa.

Anayesoma Seerah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) ataona kuwa alikuwa akifanya mzaha lakini sio mno na pasipo mahala pake. Kwa hivyo kwa msingi wa mifano iliyo mizuri mno mtu asifanye mzaha sana akaja akajuta kwa hilo.

---

mwaka 2007 uliokumbwa na utata na kusababisha ghasia.

Ghasia hizi mpya zimesababisha wasiwasi mkubwa kuhusu hali ya usalama na uwezo wa polisi kuthibiti hali katika maeneo tete.

Ghasia katika eneo hilo zilizuka kwa mara ya kwanza mwezi Agosti mwaka jana ambapo watu wa jamii za Pokomo ambao ni wakulima walipigana na jirani zao wa Orma ambao ni Wafugaji na kusababisha mauaji.

Mwezi Disemba pekee watu 45